

NATAKA NIWE NANI WAKATI WA COVID-19?



MWENYE HOFU

- NALALAMIKA MARA KWA MARA
- NASAMBAZA KILA UJUMBE NINAOLIPOKEA
- NAKASIRIKA HARAKA
- NAENEZA HISIA ZA HOFU NA HASIRA

ANAYEJIFUNZA

- NATAMBUA NA KUKUBALI HISIA ZANGU
- NATAMBUA KUWA SOTE TUNAFANYA TUWEZAVYO
- NAWACHA KUTILIA MAANANI YANAYOUMIZA HISIA ZANGU
- NAWACHA NISICHOWEZA KUDHIBITI

ANAYEJIKUZA

- NAKUBALI MABADILIKO YA MSIMU HUU
- NAWAFIKIRIA NA KUWATHAMINI WENGINE
- NAJIJALI NA KLIWAJALI WENGINE
- NAISHI SASA NA KUZINGATIA YAJAYO
- NITAKUWA MWAMINIFU JULU YA HISIA ZANGU NA NITAENEZA MATUMAINI



N/A NI MWANAFUNZI. YEYE HUTIA BIDII ILIKUYAAFIKIA MALENGO YAKE MAISHANI. ELIMU YAKE ILIKATIZIWA KIGHAFLA KWA SABABU YA JANGA LA COVID-19. KWA SASA HAENDI SHULE. N/A PAMOJA NA MARAFIKI ZAKE WAMEKUA WAKITAFUTA MBINU ZAKUKABILIANA NA HALI HII WAKIWA NYUMBANI NA WANAMATUMAINI KUWA NDOTO ZAO NA MALENGO YAO BADO YATATIMIKA.




Karibu kwenye ulimwengu wa nia!

TOMA



MUUGUZI KISULI



KEVO



ZAWADI



ELIZA



MICHI



NANA



OJ





- ❖ VIRUSI VYA KORONA VITAKUWA NASI KWA MUDA MREFU. LAZIMA SOTE TUJILINDE KWANI Yaweza kuchukua miaka kabla kukabiliwa
- ❖ VIRUSI VYA KORONA NI UKWELI. SI UTAPELI WALA UZUSHI
- ❖ TUKIJIKINGA SOTE, TUTAKUWA SALAMA ZAIDI
- ❖ HAKUNA TIBA WALA KINGA YA VIRUSI VYA KORONA KWA SASA

K →
1.5M-2M



VIRUSI VYA KORONA NI NINI?

NI FAMILIA KUBWA YA VIRUSI AMBAVYO HUSABABISHA UGONJWA KWA WANYAMA AU WANADAMU. COVID-19 NI VIRUSI VILIVYOJULIKANA HIVI KARIBUNI, AMBAVYO KWA SASA NI JANGA KUBWA LINALOATHIRI ULMWENGU MZIMA.



MUUGUZI KISULI, VIRUSI VYA
KORONA HUSAMBAZWA VIPI?



ELIZA, WAKATI MATE YA
MTU ALIYEAMBUKIZWA YAKIFIKIA
PUA, MDOMO AU MACHO YA
YULE HAJAAMBUKIZWA, KUPIGA
CHAFYA AU KUKOHOA. PIA KUPITIA
MIKONO YETU TUNAPOGUSA
MAENEO AMBAYO VIRUSI
VINAWeza KUKAA KWA MUDA
NA KUSAMBAZWA.

JE, NIFANYE NINI ILI
NISIAMBUKIZWE?



KEVO, SABUNI
HUIA VIRUSI VYA KORONA WAKATI
LITAOSHA MIKONO YAKO
SAWASAWA KUTUMIA SABUNI NA
MAJI KWA SEKUNDE 20.
PANGUSA MAENEO YOTE YA
NYUMBA KUTUMIA MAJI YA
SABUNI MARA KWA MARA.



JE, NITAJIKINGA VIPI KUTOKANA
NA VIRUSI VYA KORONA?

NANA, WEKA UMBALI SALAMA WA ANGALAU MITA MOJA UNUSU
HADI MITA MBILI KATI YAKO NA YULE MWINGINE. IWAPO WEWE
AMA YULE MWINGINE ATAKOHOA, KUPIGA CHAFYA AU
KUONGEA, VIRUSI KWA KORONA HAVITASAMBA KWA URAHISI
KUPITIA MATE. WATU WENGINE WALIOAMBUKIZWA HAWANA
DALILI. BADALA YA KUAMKUANA KWA SALAMU ZA MKONO AU
KUKUMBATIANA, AMKUANA KWA SAUTI YAKO YA FURAH.

KAA NYUMBANI. IWAPO LAZIMA UTOKE NJE, ZOEI KUVAA
BARAKOA KILA MARA KAMA IPASAVYO ILI KUJIKINGA NA
KUWAKINGA WENGINE. USIZIGUSE SEHEMU AMBAZO
ZINAWEZAKUA ZILIGUSWA NA MTU ALIYEAMBUKIZWA, UNAWEZA
KUAMBUKIZWA WAKATI UTASUGUA MACHO YAKO AU KUGUSA
USO WAKO. KUWEKA UMBALI SI UJEUJI, NI KUTULINDA SISI
SOTE.

ZAWADI, BADO UNAKUJA
KUNITEMBELEA?

HAPANA. KWA SASA,
ILI NIKULINDE LAZIMA NIENDELEE
KUKAA MBALI NAWI. NI RAHISI ZAIDI
KWA WAZEE KUKABILIWA NA VIRUSI VYA
KORONA NA NINGEPENDA UENDELEE
KUIWA HAI NA MWENYE AFYA. NANA,
WAKATI VIRUSI HVI VITAKABILIWA,
NITAKUJA KUKUKUMBATIA, KULA
CHAKULA CHAKO NA KUPATA
USHAURI WA BUSARA.

ZAWADI, NIMESIKIA KUNA TIBA HUKU KWETU. JE, NI
KWELI UKINYWA CHAI ILIYOTIWA LIMAU BILA SUKARI
ASUBUHI NA MAPEMA ITAPONYA VIRUSI VYA
KORONA?

NANA, SIO UKWELI.
NILITHIBITISHA NA MUUGUZI
KISULI KUWA HAKUNA TIBA.
MAOMBI, CHAI AU MITI SHAMBA
HAITATUKINGA KUTOKANA NA VIRUSI
VYA KORONA. WATAFITI ULIMWENGUNI
BADO WANASHUGHULIKIA CHANJO
NA PENGINE, ITAKUWA TAYARI
MWAKA WA 2021.





ZAWADI,
NINAPASWA KUOSHA
MIKONO YANGU MARA
NGAPI?



UKIGUSA MAENEO
PALE NYUMBANI ALI USO WAKO
KWA BAHATI MBAYA, PUNDE TU
UFIKAPO NYUMBANI KUTOKA NJE NA
KABLA YA KULA, OSHA MIKONO YAKO
SAWASAWA KWA SABUNI NA MAJI KWA
SEKUNDE 20. NIA, ZINGATIA KUOSHA
MIKONO YAKO KABLA HUJAGUSA
USO WAKO, MACHO
ALI BARAKOA.

JE,
NI LINI NITaweza
KUCHEZA NA MARAFIKI ZANGU?

NIA, KWA SASA,
KILA TUNAVYOENDELEA
KUKAA NYUMBANI, TUNAPUNGUZA
UWEZO WA VIRUSI VYA KORONA
KUENEA NA KUJILINDA SISI NA
WAPENDWA WETU. TUTAWEZA KUCHEZA
TENA WAKATI VIRUSI HIVI VITAKABILWA.
KUKAA NYUMBANI NI KULINDA MAISHA
YETU YA BAADAYE. TUNAWEZA
KUMPIGIA SIMU NANA KILA SIKU
JIONI ILI TUJUE
ALIVYOSHINDA.

DALILI ZA VIRUSI VYA KORONA

- HOMA, KIKOHOZI KIKAVU, NA UCHOVU
- UCHUNGU NA MAUMIVU, MSONGAMANO WA PUA, VIDONDA VYA KOO ALI KUHARA
- WATU WAZEE, NA WALE WALIO NA WANAOLUGUA MAGONJWA KAMA VILE SHINIKIZO LA DAMU, SHIDA ZA MOYO NA MAPAFU, UGONJWA WA KISUKARI, ALI SARATANI, WANaweza KABILIWA NA VIRUSI HIVI KWA URAHISI ZAIDI
- WATU WA KILA UMRI AMBAO WATAONYESHA MOJAWAPO YA HIZI DALILI WANAFAA KUTAFUTA HUDUMA ZA MATIBABU HARAKA IWEZEKANAVYO



VIRUSI VYA KORONA VINAWEZA KUISHI KWA MUDA MREFU



Pesa



Kitasa cha
mlango
/ lango



Funguo
na kufuli




Sakafu za
Boda boda
/ tukutuk na
matatu



KUMBUKA:

- Epuka kutumia pesa. Tumia pesa za rununu (Mpesa, Airtel money)
- Tumia bega / kiwiko chako kufungua mlango ukiweza, kama huwezi tumia sanitizer baada ya kugusa kwa mikono
- Epuka kugusa sakafu za boda-boda / tuk-tuk na matatu. Ikiwa utafanya hivyo, tumia sanitizer
- Tupa barakoa za kutumiwa mara moja kwenye pipa la takataka punde ikishaitumia. Osha barakoa yako ya kitambaa kwa sabuni na ulkaushe kwa hewa kavu kabla kuitumia tena
- Kuzingatia matumizi sahihi ya barakoa, hakikisha imefunika pua hadi kwa kidevu. Unapozungumza, usiitoe. Usiivae kwenye shingo



CALL 0800 721 530 FOR FREE, ANYTIME

Talk safely and privately to a professional about missed periods, period pain, forced sex or violence.



SMS 'FACTS' TO 22684, FREE

Get answers to questions you have about your periods, safe sex and emergency contraceptives – private, no judgement.



JOIN A PARENTS SUPPORT GROUP. SEND 'NIA' TO 0736 275 978

Join a tailored support group with health experts for mums-to-be, mums or parents on Mums Village.



DIAL *291# TO GET STUDY MATERIALS

Study by accessing unlimited lessons, quizzes and revision papers for upper primary and secondary school students. Enjoy the ask-a-teacher feature where you ask any academic question for only 3 bob per day using a Safaricom line.



KURIPOTI VISA VYA KORONA, PIGA SIMU
NAMBARI 719, BILA MALIPO



@YanguNia



@niayanguke



@NiaYanguKe

To order for print comics, email nia@zanaafrica.org

